# Kupunguza hatari za vifo kwa watoto wagonjwa na wenye utapiamlo

Hatari ya kufa wakati na baada ya magonjwa ya utotoni kama vile kuhara, nimonia, maambukizo mengine na malaria ni kubwa katika nchi za kipato cha chini na cha kati. Mtandao wa Childhood Acute Illness & Nutrition ("CHAIN") unataka kuboresha malezi ya watoto na kuelewa mambo yanayoongeza uwezekano wao kufa. Utafiti wa CHAIN:


- Uliandikisha watoto wa umri wa miezi 2-23 waliokuwa wagonjwa waliolazwa katika hospitali tisa katika nchi nne za Afrika na mbili za Asia Kusini.
- Ulikusanya habari juu ya hali ya kliniki, lishe na hali ya jamii ya watoto.
- Ulifuatilia watoto wakati walipokuwa hospitalini na kwa miezi sita baada ya kutoka

Utafiti wa CHAIN Study ulifanikishwa na watoto na walezi wao kwa watoto na walezi wao ambao walishiriki Kwa hiari katika utafiti, Ushirikishaji na usaidizi kutoka kwa wanajamii na Wizara Za Afya za mitaa, na uongozi wa wafanyikazi wa afya na watafiti kutoka duniani kote.


## MATOKEO YA UTAFITI WA CHAIN - ULIOELEKEZWA KWA JAMII

### HATARI KUU NA MATATIZO


Hospitali / vifo baada ya kutoka



Watoto wagonjwa ambao ni wembamba sana (walio na utapiamlo) wanauwezekano wa kufa hospitalini au baada ya kutoka mara, tano zaidi ikilinganishwa na watoto wasio wembamba.




Baada ya kutoka hospitalini, watoto wanaweza kuonekana na nafuu kutokana na ugonjwa wao lakini kubaki dhaifu na rahisi kuambukizwa. CHAIN ilipata nusu ya vifo vyote vya utafiti vilitokea baada ya kutoka.



Watoto wengine wagonjwa huondoka hospitalini kabla ya kuwa tayari kwa kutolewa. CHAIN ilipata watoto waliotoka hospitalini kinyume na ushauri wa daktari walikuwa na uwezekano wa kufa mara mbili zaidi.

Mambo Yanayochangia Afya



Watoto wenye utapiamlo sio tu wanateseka kwa kukosa chakula. Lishe yao, Afya, na hatari ya kufa huathiriwa na magonjwa ya msingi na mazingira ya kijamii na mazingira ya nyumbani kwa walezi wao.


### RUHUSA YA KUINGIA

UTUNZAJI WA PAPO HAPO

KUTOKA

KURUDI NYUMBANI

### UJUME MUHIMU




Wapeleke watoto waliokonda au wasiokua vizuri kwenye huduma ya matibabu ili kupunguza uwezekano wa magonjwa kama vile nimonia na kuhara.




Fuata ushauri wa daktari wako kuhusu wakati unaofaa kuondoka hospitalini ili kusaidia kuzuia vifo baada ya kutoka. Unapoondoka, muulize daktari wako ni ziara gani za kufuatilia zinazohitajika kwa mtoto wako, na jinsi ya kutambua dalili za hatari:

- Kusinzia
- Kutoweza kula vizuri
- Kupumua kwa shida/ugumu wa kupumua
- Kutapika kwa kuendelea





Mara unaporudi nyumbani, watoto bado wako katika hatari hata kama wanaonekana wakiwa wamepona kutokana na ugonjwa. Ukiona dalili za hatari tafuta matibabu kwa mtoto wako.



Wazazi na Walezi wenye afya njema hufanya watoto kuwa na afya njema.

Chukua fursa yoyote uwezayo kutunza afya yako na ya familia yako, ikijumuisha kile unachokula na kutafuta matibabu unapohitaji.

THE GLOBAL HEALTH NETWORK
Enabling research by sharing knowledge
SickKids Centre for Global Child Health
Centre MURAZ